# Njia ya Matumaini:

## Wasichana Wakimbizi Waliobaleghe wa Kongo katika Kambi ya Wakimbizi ya Nyarugusu, Tanzania

Utafiti Uliofanywa na Tume ya Wakimbizi ya Wanawake

Januari 2013

*RIPOTI YA WACHANGIAJI WA JAMII*

**SISI NI KINA NANI?**

Tume ya Wakimbizi ya Wanawake (WRC) ni shirika la utafiti na utetezi lilio New York, Marekani. Lengo letu ni kuboresha maisha na kulinda haki za wanawake, watoto na watu wachanga waliotawanywa kwa sababu ya vita, mashtaka au janga la asili. Tunatetea mabadiliko ya sheria, sera na mipango inayoathiri watu walioathiriwa na mizozo au migogoro.

**KWA NINI TULIKUJA TANZANIA?**

WRC ilisafiri katika Eneo la Kigoma la Tanzania ili kuzungumza na wasichana wakimbizi waliobaleghe wenye umri wa 10-16 kwenye Kambi ya Wakimbizi ya Nyarugusu. Tulizungumza na wasichana kuhusu matatizo yao na kile ambacho kingeweza kufanywa ili kuboresha maisha yao. Lengo lilikuwa kuhakikisha kuwa uwakala unaofanya kazi na wakambizi unaelewa hali ya kipekee ya wasichana waliobaleghe. Tutatumia matokeo ya utafiti wetu ili kuhimiza uwakala unaofanya kazi na wakimbizi kuandaa mipango inayosaidia kulinda wasichana waliobaleghe.

**TULIFANYA NINI WAKATI WA ZIARA YETU?**

Wafanyakazi wawili kutoka kwenye WRC walikutana na wasichana 36 wakimbizi waliobaleghe Kongo, wavulana 10 waliobaleghe, viongozi 16 wa jamii wanawake na wanaume, kina mama tisa na kina baba wawili wa wasichana waliobaleghe, na wafanyakazi 15 wa uwakala unaofanya kazi kwenye Kambi ya Wakimbizi ya Nyarugusu. Tulizungumza na kila mtu ili kujua kile ambacho wasichana wanakihitaji ili wakue kama kina mama wachanga wenye afya, wasiodhulumiwa na wanaoweza kujitegemea..



Wasichana wakimbizi wa Kongo wakishiriki katika zoezi kwenye ramani kuhusu usalama, wakifafanua kule wanakohisi kuwa salama na kusiko salama wanapofanya kazi zao za kila siku.

**MUKTADHA WA TANZANIA**

Tanzania imetia sahihi Mkutano wa 1951 Unaohusiana na Hali ya Wakimbizi na Itifaki yake ya 1967. Mkutano na Itifaki vinafafanua mkimbizi ni nani na haki za watu wanaopewa hifadhi. Pia imetia sahihi Shirika la Mkutano wa Umoja wa Afrika (OAU). Lakini maisha ya mkimbizi wa Kongo, *haswa msichana mkimbizi,* bado ni magumu sana. Kwa nini?

1. Wakimbizi hawana haki ya kufanya kazi Tanzania. Huku ni kumaanisha kuwa wanaishi kwa kufanya kazi za jua kali ambazo ni za malipo duni na hatari wakati mwingine. Wakati familia inapokosa mapato ya kutosha, wasichana hulazimika kufanya kazi nyumbani au nje ili kusaidia familia. Huku ni kumaanisha kuwa hulazimika kuacha shule kila mara. Kazi nje ya nyumbani zinaweza kuwa hatari; wasichana huhisi kukosa usalama wanaposafiri nje kinyume cha sheria ili kutafuta pesa.

2. Ingawa watoto wakimbizi wana haki sawa za elimu kama watoto wa Tanzania, usajili wa shule za wasichana wakimbizi uko chini na viwango vya wanaoacha shule ni vya juu. Wakati mwinginge wasichana hupata mimba au kuozwa mapema, na basi kuacha shule. Hii inaathiri vibaya hatima yao na maisha watakayoishi kama watu wazima.

**TULIJIFUNZA NINI?**

1. Kuna ukosefu wa usalama ndani na nje ya kambi na mara kwa mara wasichana huhisi kutokuwa na usalama wanapofanya kazi zao za kila siku. Wasichana wanasafiri mbali zaidi ya kambi kutafuta kuni, kitu kinachowahatarisha sana kwa madhara ya kimwili.
2. Wasichana wana nafasi chache za kupata mbinu za maish kwa sababu mara kwa mara wanashughulika sana kufanya kazi za familia au kushiriki katika shughuli za kutafuta riziki ndani na nje ya kambi.
3. Viwango vya kuwacha shule kwa wasichana ni vya juu kwa sababu ya umaskini na ukosefu wa vitu vya msingi kama vile sabuni ya kufua nguo na pesa za kununua vifaa vya shule. Pia wasichana wako katika hatari ya kuacha shule kwa sababu wanadhulumiwa kingono na vurugu, kupata mimba, au kulazimishwa kuolewa.
4. Wasichana huwa na muda mchache wa kucheza au kutangamana na wengine. Wanakosa msaada kutoka kwa marika yao na wana mifano michache ya kuiga ili kuwasaidia.
5. Wasichana hukosa nafasi za kazi zilizo salama. Wasichana wote tuliozungumza nao walikuwa wakishiriki katika baadhi shughuli nyingine za maisha zisizo salama, mara kwa mara wakiwa katika hatari ya kuenda nje ya kambi kwa biashara ndogo ndogo, vibarua au kufanya kazi katika shamba la mwenyeji. Nafasi za kujifunza mbinu wakati wa likizo ni chache. Mara kwa mara hupatikana tu kwa vijana wakubwa au wanawake, na wasichana wachache hushiriki kwazo.

6. Mashirika Yasiyo ya Serikali ya Karibu na ya Kimataifa yanafanya kila yawezalo kutoa huduma muhimu kwa wakimbizi. Lakini hakuna uhakika ikiwa yanafikia wasichana waliobaleghe kwa sababu data za programu hazikusanywi maalum kwa wasichana.



Wasichana wa shule ya upili wakitembea kwa usalama kuelekea nyumbani pamoja kutoka shuleni.

**TUNAPENDEKEZA NINI?**

1. <u>Tume ya Wakimbizi ya Umoja wa Mataifa (UNHCR) inastahili:</u>

- ✓ kutetea ikiwa ni pamoja na Wizara ya Mambo ya Nyumbani kuruhusu kuendelea kwa uzalishaji wa mapato ya wakimbizi na shughuli za masoko ndani na nje ya kambi;
- ✓ kutoa kipaumbele kwa maendeleo ya vyanzo vingine vya kawi ya mafuta ya kupika na majiko ya mafuta ya kupika vizuri ili kuweka wanawake na wasichana salama na kutunza mazingira;
- ✓ kufanya kazi kwa karibu na watoa huduma, uongozi wa kamati ya kambini na polisi ya taifa kuleta usalama wa kujilinda (*sungusungu).*

2. <u>Watoa huduma na mashirika ya jamii ya wakimbizi yanastahili:</u>

- ✓ kushauriana na wasichana wenyewe na wanajamii, ikiwa ni pamoja na watunzaji wa wasichana na wavulana, katika kuunda, kutekeleza na kufuatilia programu;
- ✓ kutia nguvu elimu ya kawaida kwa wasichana ili wawe na nafasi nyingi za kupata mbinu za maisha, likizo na kuunda mitandao ya jamii na marika yao;
- ✓ kuhakikisha kuwa programu zilizopo zinasaidia kushiriki zaidi kwa wasichana na kuwawezesha kubaleghe bila shida ili wasichana wasione taabu wanapoomba msaada;
- ✓ wakati wa kukusanya data za programu, kuhakikisha kuwa wasichana wamehesabiwa kwa kwa kuchukua malezo yasiyojumuishwa ya jinsia na umri.

**TUTAFANYA NINI SASA?**

Tume ya Wakimbizi Wanawake itashiriki matokeo na mapendekezo haya ili kuboresha hali ya wasichana wakimbizi wa Kongo, Tanzania. Tunapanga kuongoza mradi mdogo kupitia mshirika wa karibu Nyarugusu ili kujaribu kuweka programu katikati kuimarisha usalama wa wasichana.

Unaweza kusoma ripoti yetu kamili na usambazaji wetu katika *Njia ya Matumaini: Wasichana Wakimbizi Waliobaleghe katika Kambi ya Wakimbizi ya Nyarugusu, Tanzania kwenye* http://wrc.ms/TvjDMy. Tafadhali tufahamishe iwapo ripoti hii ilikufaa kupitia info@wrcommission.org.

**Shukrani**

Tunawashukuru wasichana wakimbizi waliobaleghe, wavulana na viongozi wa jamii waliotumia muda na sauti zao katika utafiti huu.

Ripoti hii iliandikwa na Kathryn Paik.

Ripoti hii ilifanikishwa kupitia ufadhili wa pesa wa Wakfu wa Familia wa Frankel na Wakfu wa Oak.

© 2013 Tume ya Wanawake Wakimibizi

Tume ya Wanawake Wakimbizi
122 East 42nd Street
New York, NY 10168-1289
212.551.3115
info@wrcommission.org

www.womensrefugeecommission.org